

Mpango wa Usaidizi wa Kujifunza kwa Kina kwa COVID

Habari kwa wazazi na walezi

Kuhusu Mpango wa Usaidizi wa Kujifunza kwa Kina kwa COVID

Mpango wa Usaidizi wa Kujifunza kwa Kina kwa COVID (COVID Intensive Learning Support Program (CILSP)) hutoa mafunzo ya kikundi kidogo kwa wanafunzi wanaohitaji zaidi kote shule za msingi, sekondari na za kitaalam za NSW.

Mpango huu ni juhudi za pamoja kati ya Idara ya Elimu ya NSW, Shule za Katoliki za NSW na Muungano wa Shule za Kujitegemea za NSW.

Mpango huu umeanzishwa ili kusaidia wanafunzi ambao kujifunza kwao kumeathiriwa na vipindi virefu vya kujifunza kutoka nyumbani kwa sababu zaidi ya janga la COVID-19. Mpango huo huzingatia kusoma, kuandika na kuhesabu.

Kila shule inatengeneza mpango wake yenyewe kutegemea mahitaji ya wanafunzi wao na inasimamia mpango kuajiri walimu waliofunzwa maalum na waelimishaji wengine kama vile wahadhiri wa vyuo vikuu na walimu wa shule za chekechea. Masomo hayo ya kikundi kidogo yanaweza kufanyikwa kabla au baada ya masaa ya shule au wakati wa masaa ya shule.

Jinsi mpango huu unafanya kazi

Kupitia mpango wa usaidizi wa kujifunza kwa kina kwa COVID, shule zinatolewa na ufadhili kuajiri waelimishaji ziada ambao wanatoa mafunzo ya kikundi kidogo kwa wanafunzi.

Kwa kushirikiana na mkuu wa shule na kutumia tathmini mbalimbali, mwalimu wa darasa anaamua ni watoto gani watafaidika kutoka mafunzo ya kikundi kidogo.

Kuingizwa kwa kila mtoto katika mpango ndipo kunazungumzwa na wazazi au walezi wake na mpango wa kufundisha unatayarishwa. Maendeleo ya mtoto yanaangaliwa kila mara na mawasiliano na wazazi na walezi yanadumishwa.

Vipengele muhimu vya mpango

- Wanafunzi katika kila shule ya Serikali ya NSW wameungwa mkono na mpango huo. Katika 2021 jumla ya wanafunzi 265,000 waliungwa mkono.
- Mafunzo ya kikundi kidogo hutolewa na waelimishaji wa ziada - ikiwa ni pamoja na walimu wa kawaida na wa muda, walimu wastaafu, na walimu wanafunzi. Walimu wa ziada wanafanya kazi karibu na walimu wa darasa kuhakikisha mafunzo yanalengwa kwa mahitaji ya wanafunzi.
- Mafunzo huzingatia kusoma, kuandika na kuhesabu.
- Timu ya waelimishaji wataalamu na katibu huunga mkono na huongoza shule katika kutekeleza mpango huo.
- Mafunzo ya kikundi kidogo yanahusu msaada wa ziada wa ufundishaji na ujifunzaji kwa vikundi vya wanafunzi 2 hadi 5. Wanafunzi wanafundishwa mara kwa mara kwa muda ulioamuliwa mapema kwa nia ya kutilia mkazo mafundisho ya darasani.

Kuhusu Mpango wa Usaidizi wa Kujifunza kwa Kina kwa COVID na mtoto wako

Mwalimu wa mtoto wako atawasiliana nawe, kama akiona mpango ungefaidika kwa mtoto wako. Ikiwa unataka kujua zaidi kuhusu mpango tembelea ukurasa wa tovuti ya Mpango wa Usaidizi wa Kujifunza kwa Kina kwa COVID ([COVID Intensive Learning Support Program webpage](#)). Ikiwa unahitaji maelezo zaidi, zungumzia mpango huu na mwalimu wa mtoto wako.

Huduma ya Mkalimani ya Simu

Ikiwa ukihitaji habari zaidi tafadhali pigia simu mkuu wa shule yako. Kama unahitaji mkalimani kukusaidia na swali lako tafadhali pigia simu kwenye Huduma ya Mkalimani ya Simu kwenye 131 450 na omba kwa mkalimani wa lugha yako. Mwambie operata nambari ile ya simu unayotaka kupiga simu, na operata atapata mkalimani kwenye simu kukusaidia na mazungumzo, Hutatozwa kwa huduma hii.